TANZANIA ELECTION MONITORING COMMITTEE

TEMCO

REDET - LEAD AGENCY OF TEMCO

TAARIFA YA AWALI KUHUSU UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA MWAKA 2015

IMETOLEWA NA

TIMU YA UANGALIZI WA UCHAGUZI YA TEMCO

OKTOBA, 2015

Orodha ya vifupisho

ACT-Wazalendo	Alliance for Change and Transparency
ADC	Alliance for Democratic Change
BVR	Biometric Voter Registration
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CEMOT	Coalition on Election Monitoring and Observation in Tanzania
CHADEMA	Chama Cha Demokrasia na Maendeleo
CUF	Civic United Front
EMB	Election Management Body
EOC	Election Observation Centre
ICT	Information Communication Technology
ID	Identity Card
LHRC	Legal and Human Rights Centre
LTOs	Long Term Observers
NCCR-Mageuzi	National Convention for constitutional Reforms
NDI	National Democratic Institute
NEC	National Electoral Commission
NIDA	National Identification Authority
NLD	National League for Democracy
OMR	Optical Mark Recognition
OMR	Optical Mark Recognition
OSIEA	Open Society Initiative for Eastern Africa
OTEP	Observation of Tanzania Electoral Processes
PNVR	Permanent National Voter Register
REDET	Research and Education for Democracy in Tanzania
STO	Short Term Observer
TANU	Tanganyika African National Union
TACCEO	Tanzania Civil Society Consortium for Election Observation
TCD	Tanzania Centre for Democracy
TEMCO	Tanzania Election Monitoring Committee
TLP	Tanzania Labour Party
UDP	United Democratic Party
UKAWA	Umoja wa Katiba ya Wananchi (Defenders of the Peoples' Constitution)
USAID	United States Agency for International Development
VIC	Voter Identity Card
ZEC	Zanzibar Electoral Commission

1. Utangulizi

Mwaka 2015 Tanzania ilifanya uchaguzi wa tano baada ya nchi kurejea mfumo wa ushindani wa siasa, ulioasisi mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kutoka mwaka 1965 mpaka mwaka 1990 ni chama kimoja tu (TANU na CCM kutoka 1977) kilichoshiriki katika chaguzi kuu Tanzania Bara na Zanzibar. Baada ya kurejea mfumo wa vyama vingi vya siasa, chaguzi zimekuwa zikivutia ushiriki wa vyama vingi vya siasa.

Mwaka 1995, vyama vinne vya siasa vilisimamisha wagombea urais na vyama 13 viliweka wagombea ubunge. Vilevile mwaka 2000 vyama vinne vya siasa vilisimamisha wagombea urais na vyama 13 viliweka wagombea ubunge. Mwaka 2005 vyama 10 vya siasa vilikuwa na wagombea urais wakati vyama 18 vilishiriki uchaguzi wa wabunge. Mwaka 2010 vyama saba vilikuwa na wagombea urais wakati vyama 18 viliweka wagombea ubunge. Mwaka 2015 vyama nane vya siasa vilikuwa na wagombea urais ambapo vyama 22 viliteua wagombea ubunge. Hata hivyo, vyama vinne, CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD viliunda umoja na kukubaliana kugawana na kuachiana majimbo ya uchaguzi katika ngazi zote: urais wa Jamhuri ya Muungano, urais wa Zanzibar, ubunge, ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, na udiwani.

Taarifa hii ya awali ina lengo la kutoa tathmini ya uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2015 kama inavyoangaziwa na ripoti za waangalizi wa uchaguzi wa TEMCO waliotawanywa nchi nzima. Taarifa hii ya awali inaangazia matokeo ya uangalizi wa TEMCO ikiwa na lengo la kusaidia kuimarisha asasi za uchaguzi ili kuboresha michakato ya chaguzi siku zijazo.

Taarifa hii ya awali ina sehemu kuu kumi. Sehemu ya kwanza ni utanguzi. Sehemu ya pili inagusia muktadha wa kisiasa na mazingira ya uchaguzi. Sehemu ya tatu na nne zimejikita katika njia za utafiti pamoja na mifumo ya kisheria na kiasasi inayotawala chaguzi za Tanzania. Masuala yahusuyo usimamizi wa uchaguzi yameelezewa katika sehemu ya tano. Sehemu ya sita inaongelea elimu ya mpiga kura mahsusi kwa uchaguzi mkuu. Sehemu ya saba ni tathmini ya ujumla ya uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2015. Sehemu ya nane ni mahsusi kwa ajili ya uchaguzi wa Zanzibar ambao umeonekana kugubikwa na sintofahamu. Sehemu ya tisa inahitimisha taarifa na kutoa mapendekezo. Sehemu ya mwisho ni shukrani kwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi waliotoa msaada wa hali na mali kufanikisha zoezi la uangalizi wa uchaguzi. Katika kipindi kifupi kijacho TEMCO itatoa taarifa yake kamili yenye matokeo ya uangalizi wake wa uchaguzi wa mwaka 2015.

2. Muktadha wa kisiasa na mazingira ya uchaguzi

Kipindi cha kuelekea uchaguzi wa mwaka 2015 kiligubikwa na matukio mengi ya kisiasa, makubwa kati ya hayo ni haya yafuatayo:

i. Mgawanyiko wa wazi wa wapiga kura na wahusika wakuu wa siasa za Tanzania juu ya Katiba Inayopendekezwa. Chama tawala CCM na wafuasi wake waliunga mkono Katiba Inayopendekezwa wakati wapinzani chini ya mwavuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) walipinga Katiba Inayopendekezwa. Maeneo yaliyoleta mvutano yalihusu muundo wa muungano. Wakati CCM ikipendelea mfumo wa sasa wa serikali mbili, UKAWA walipigia chapuo serikali tatu;

ii. Uamuzi wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ukiundwa na vyama vinne yaani, CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD kugawana na kuachiana majimbo ya uchaguzi katika ngazi zote wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015;

iii. Kushindwa kutekelezwa kwa "makubaliano ya kiungwana" kati ya Rais Jakaya Kikwete na TCD yakilenga kuboresha uwazi na haki katika uchaguzi wa mwaka 2015, ikiwemo: (i) kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi; (ii) ushiriki wa wagombea binafsi katika uchaguzi; (iii) ushindi wa asilimia 50%+1 ili kutangazwa kuwa rais badala ya mfumo wa "wengi wape"; (iv) uwezekano wa kupinga matokeo ya kura ya urais mahakamani; na, (v) kusitishwa kwa mchakato wa katiba mpya mpaka baada ya uchaguzi wa mwaka 2015;

iv. Chama kimoja, CCM, kutamalaki siasa za Tanzania tangu uhuru mwaka 1961. Chama tawala kimekuwa kikishinda chaguzi zote za rais na kuendelea kupata viti viti vya ubunge, baraza la wawakilishi na serikali za mitaa;

v. Kasi ndogo ya ukuaji wa demokrasia ndani ya vyama vya siasa, kilele chake ikiwa kukosa uvumilivu wa fikra pinzani kulikopelekea baadhi ya wanachama kufukuzwa na kulazimika kuunda vyama vingine vya siasa. Vyama vipya viwili, ACT-Wazalendo na ADC, ni matokeo ya migogoro ndani ya CHADEMA na CUF;

vi. Ushindani mkali kati ya wanachama wa CCM waliowania uteuzi wa kusimama katika nafasi mbalimbali za kuchaguliwa. Mathalani, wagombea 42 wakiwemo mawaziri waliomba uteuzi katika nafasi ya urais;

vii. Matokeo yasiyotarajiwa ndani ya vyama vya siasa hasa CCM na vyama vinavyounda UKAWA hasa CHADEMA na CUF. Ndani ya CCM, Edward Ngoyai Lowasa (waziri mkuu aliejiuzulu); Frederick Tluway Sumaye (waziri mkuu mstaafu), Kingunge Ngombale Mwiru, naibu waziri mmoja na wenyeviti watatu wa CCM mkoa walijitoa ndani ya CCM na kujiunga na CHADEMA. Edward Lowassa aliteuliwa kuwa mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA akiungwa mkono na vyama vinavyounda UKAWA. Ndani ya CHADEMA na CUF, baadhi ya viongozi wa juu waliamua kujitoa katika vyama vyao wakipinga hatua ya UKAWA kuwapokea wagombea walioachwa na CCM. Katibu Mkuu wa CHADEMA aliyesimama katika uchaguzi wa mwaka 2010 na akitarajiwa kusimama tena kwa tiketi ya chama mwaka 2015 alijiuzulu. Pia Mwenyekiti wa CUF aliamua kujiuzulu na kubaki kuwa mwanachama wa kawaida;

viii. Kukosekana uwiano wa nguvu kati ya vyama vya siasa. Katika uchaguzi wa mwaka 2010 CCM ilipata viti 186 katika bunge la Jamhuri ya Muungano na viti 28 katika baraza la wawakilishi, CUF ilikuwa na viti 24 katika bunge la Jamhuri ya Muungano na 22 katika baraza la wawakilishi. Vyama vingine vilikuwa na viti kama ifuatavyo: CHADEMA-23, NCCR-Mageuzi-4, UDP-1 na TLP-1. Hii pia ilikuwa na athari katika kupata rasilimali fedha kutoka serikalini. Kadri chama kinavyokuwa na viti vingi bungeni ndivyo kinavyopata ruzuku zaidi kutoka serikalini.

Kwa ujumla, TEMCO ilitiwa moyo na mazingira ya kisiasa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015 kwa kuona kuwa nchi iliendelea kubaki salama huku vyama vya siasa na wagombea, na jamii kwa ujumla wakionyesha uvumilivu wa hali ya juu. Hii iliwawezesha Watanzania kutekeleza haki yao ya msingi na uhuru wa kuchagua kwa mujibu wa katiba. Mazingira ya uchaguzi yalikuwa shwari kiasi cha kuwezesha uchaguzi wa kidemokrasia kufanyika.

3. Mifumo ya kisheria na kiasasi

Mfumo wa kisheria unaotawala chaguzi za Tanzania unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 pamoja na marekebisho yake inatoa mwongozo wa ufanyikaji wa uchaguzi wa rais wa Jamhuri ya Muugano na ubunge. Uchaguzi wa serikali za mitaa hufanyika chini ya Sheria ya Serikiali za Mitaa ya mwaka 1979 pamoja na sheria nyingine. Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya 2010

pia ina vipengele vinavyohusu ugharimiaji wa uchaguzi, ikiwa na lengo la kudhibiti matumizi wakati wa uchaguzi.

Chaguzi za Zanzibar huongozwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1984 pamoja na marekebisho yake.

Kuna tume mbili za uchaguzi Tanzania. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kusimamia chaguzi za Jamhuri ya Muungano. Wajumbe wa tume huteuliwa na rais wa Jamhuri ya Muungano na wanatekeleza majukumu yao kama inavyoelekezwa katika sheria za uchaguzi. Baadhi ya wadau wa uchaguzi hawaridhishwi na sheria zinazotawala chaguzi Tanzania. Kuna hisia na mashaka kuwa sheria ina upungufu, mkubwa zaidi ikiwa:

i. Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina mamlaka ya kutosha ya kutekeleza majukumu yake bila upendeleo. Mashaka haya yanatokana na ukweli kuwa Mwenyekiti wa Tume, makamu wake, makamishna, na mkurugenzi wa uchaguzi huteuliwa na rais ambaye pia ni mwenyekiti wa chama cha siasa na wakati mwingine mgombea katika nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano;
ii. Tume haina wafanyakazi na maafisa wake mahsusi ukiacha wale walioko makao makuu Dar es Salaam. Inategemea kiasi kikubwa wafanyakazi wa serikali ambao huwepo kwa ridhaa ya rais. Utii wa wafanyakazi hawa uko kwa mwajiri wao na sio Tume;
iii. Sheria hairuhusu mgombea binafsi, ikiwataka wagombea kupata uteuzi wa vyama na hivyo kuminya haki za kisiasa na za kiraia;
iv. Sheria imewabagua Watanzania waishio nje ya nchi kujiandikisha ili kupiga kura na pia kusimama kama wagombea;
v. Pamoja na kutokuelezwa kinagaubaga na sheria kiuhalisia wafungwa wanaotumikia vifungo vya chini ya miezi sita na wagonjwa wanaolazwa hospitali hukosa haki ya kupiga kura.
vi. Kukosekana miundo na taratibu za kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010.

Kwa ujumla, sheria zinazotawala chaguzi za Tanzania sio za kikatili wala za kuchukiza. Kwa ujumla zinatoa haki ya kupiga na kupigiwa kura. Sheria na asasi zinakaribia kwa kiasi kikubwa viwango vinavyokubalika vya kimataifa. Hata hivyo kuna vipengele katika sheria ambavyo vinahitaji marekebisho makubwa ili kuongeza imani ya wadau wa uchaguzi na ili kufikia uchaguzi ambao ni wa kuaminika, huru na wa haki.

4. Njia na mbinu za kukusanya takwimu na taarifa

Utazamaji wa uchaguzi wa mwaka 2015 ulifanyika katika hatua mbili zinazotemegeana. Hatua ya kwanza ilihusu utazamaji wa mchakato wa uandikishaji wa wapiga kura ambapo kwa mara ya kwanza mfumo wa kidijitali wa BVR ulitumika. Hatua ya pili ilihusisha utazamaji wa michakato mingine katika mzunguko wa uchaguzi.

Katika hatua ya kwanza TEMCO ilitoa mafunzo na kuweka waangalizi wa muda mrefu yaani Long Term Observers 163 kwa siku 21 kuangalia zoezi la uandikishaji wa wapiga kura kwa kutumia mfumo wa BVR katika halmashauri 140, kata 1,216 na vituo vya kuandikishia wapiga kura 9,728 Tanzania Bara; na wilaya 11, Shehia 88 na vituo vya uandikishaji 704 Zanzibar. Zoezi la uandikishaji wa wapiga kura liliangaliwa katika halmashauri za wilaya zilizopo maeneo ya mipakani ikiwemo mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Mbeya, Mtwara, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara na miji yote mikuu. Seti mbili za madodoso zilitumika kukusanya takwimu kuhusu zoezi la BVR.

Katika hatua ya pili jumla ya waangalizi wa muda mrefu 150 walipewa mafunzo na kupangiwa majimbo ya kuangalia na kutakiwa kukaa huko kwa siku 44 kuangalia kampeni na wakati huohuo kukusanya taarifa za matukio muhimu yaliyotokea kabla ya kampeni. Matukio haya ni yale yanayohusu mgawanyo wa majimbo na kata, pamoja na uteuzi wa wagombea ndani ya vyama na wa Tume. Watazamaji walitumia seti mbili za dodoso: (i) Dodoso la Kituo cha Uangalizi wa Uchaguzi (Election Observation Centre-EOC) cha CEMOT ambalo lilikusanya taarifa za kabla ya uchaguzi. Taarifa zilitumwa kwenye mtandao kwa kutumia *Magpi*; na (ii) dodoso la TEMCO ambalo lilikuwa na maswali ya wazi na yaliyofungwa kwa ajili ya kupata habari na takwimu za kampeni kwa ajili ya ripoti ya mwisho. Siku ya uchaguzi waangalizi waliangalia upigaji kura, kuhesabu kura, utangazaji wa matokeo na matukio baada ya uchaguzi.

TEMCO pia iliweka waangalizi wa Muda Mfupi (Short Term Observers-STOs) 7,350 katika vituo vya kupigia kura katika majimbo 150 Tanzania Bara (6,646) na Zanzibar (704). Waangalizi wa muda mfupi walikuwa na seti mbili za madodoso: (i) Dodoso la CEMOT la kukusanya taaarifa za siku ya uchaguzi ambalo lilikuwa na maswali 69 na kutumwa kwa kutumia ujumbe mfupi wa simu. (ii) Dodoso la TEMCO lililokuwa na maswali ya wazi na yaliyofungwa kuhusu siku ya upigaji kura. Taarifa zilifanyiwa uchambuzi na zilitumika katika kuandaa ripoti mbalimbali za TEMCO.

Usaili na maafisa wa uchaguzi katika ngazi mbalimbali pamoja na viongozi wa vyama vya siasa ulitumika pia kupata taarifa za michakato ya uchaguzi. Waangalizi wa muda mrefu pamoja na wachambuzi wa TEMCO walipitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza chaguzi Tanzania.

Kwa minajili ya taarifa hii, waangalizi wa muda mrefu na wa muda mfupi walitakiwa kufanya tathmini ya haraka juu ya uteuzi wa wagombea, kampeni pamoja na matukio ya siku ya kupiga kura na mara baada ya matokeo kutangazwa na kuzituma makao makuu ya TEMCO, Dar es Salaam. Tathmini hii imetoa mwelekeo wa michakato mitatu ya uchaguzi na imeiwezesha TEMCO kubashiri kiwango ambacho uchaguzi mzima unaweza kuchukuliwa kama "*huru na wa haki*". Watazamaji walitoa alama kwa kila moja ya michakato ya uchaguzi kama ifuatavyo:

i. 0% au alama F: uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambayo imeshindwa kabisa katika usimamizi, utii wa sheria, kanuni na taratibu na haki kiasi kwamba uchaguzi hauwezi kuhesabiwa kuwa umekamilika. TEMCO huupa mchakato kama huu cheti "*uchaguzi uliovia*".
ii. 1-39% au alama E: uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) iliyokabiliwa na matatizo lukuki ya kiutendaji pamoja na ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu kiasi kwamba wadau wakuu (wapiga kura, wagombea, na vyama) wanakataa matokeo. Mchakato kama huu hupewa cheti cha "*uchaguzi uliovurugwa*".
iii. 40-49% au alama D: mchakato wa uchaguzi uligubikwa na vitendo vya vurugu, vitisho, upendeleo, rushwa, n.k. Cheti stahiki kwa mchakato kama huu ni uchaguzi ambao "*sio huru na wala sio wa haki*".
iv. 50-59% au alama C: uchaguzi uliruhusu ushiriki wa wadau (wapiga kura, wagombea, vyama na wengineo) lakini chama tawala na vyama vikubwa vilikiuka taratibu bila kuchukuliwa hatua. Hii ni kusema uchaguzi ulikuwa "*huru lakini si wa haki*".
v. 60-79% au alama B: uchaguzi ambao kwa jumla ni huru na wa haki, lakini bado kuna upungufu ambao unaweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapiga kura). TEMCO hutoa cheti cha uchaguzi "*huru na wa haki lakini wenye shaka*".

vi. 80% au zaidi au alama A: Ni uchaguzi safi na wa kiungwana ambao una upungufu wa kawaida usioweza kuathiri matokeo ya uchaguzi. Unaostahili cheti cha uchaguzi "*safi, huru na wa haki*".

5. Usimamizi wa uchaguzi

Usimamizi wa uchaguzi ni jukumu la Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Kuelekea uchaguzi wa mwaka 2015 Tume ilikamilisha shughuli mbalimbali ambazo zilitoa mwelekeo wa uchaguzi. Baadhi ya shughuli hizo ni: (i) manunuzi na usambazaji wa vifaa, vikiwemo vya BVR; (ii) kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura kwa kutumia mfumo wa BVR. Zoezi hili liliwalazimisha wote wenye sifa za kupiga kura kuhuisha taarifa zao na kurejesha kadi zao za awali za kupigia kura zilizotayarishwa kwa mfumo wa OMR; (iii) kutoa mafunzo kwa maafisha chaguzi katika ngazi za taifa, mkoa na wilaya; na (iv) kuandaa na kusambaza kanuni za maadili ya uchaguzi kwa vyama vya siasa, wagombea na waangalizi uchaguzi.

Kwa ujumla Tume ilitimiza majukumu yake kikamilifu na kwa namna ambayo ilijaa weledi ingawa ilikabiliwa na upungufu wa rasiliamali pamoja na kufanya kazi kwa shinikizo kubwa kutoka kwa wadau wa uchaguzi.

6. Tathmini ya michakato ya uchaguzi

6.1 Kugawanya majimbo

Majimbo mapya 25 yalianzishwa na hivyo kufanya idadi ya majimbo kuongezeka kufikia 264 kutoka 239 ya awali. Kata ziliongezwa kutoka 3,339 mwaka 2010 mpaka 3,957 mwaka 2015. Ugawaji wa majimbo ulifanywa kwa umakini na ulikuwa wazi, kwa kutumia taratibu huru na zilizonyooka kwa mujibu wa sheria. Baadhi ya vigezo vilivyotumika ni wingi wa watu na ukubwa wa eneo la kijiografia au kiutawala.

Hakukuwa na malalamiko kutoka kwa wadau wa uchaguzi juu ya hatua hii ya Tume. Matokeo ya watazamaji wa TEMCO hayaonyeshi chembechembe za hila za upendeleo katika kupanga majimbo. TEMCO inaipongeza Tume kwa kufanya mgawanyo wa majimbo kwa weledi na kwa namna ambayo ilikubalika na kuwaridhisha wadau wote.

6.2 Uandikishaji wa wapiga kura

TEMCO ilibaini kuwa Tume iliandikisha jumla ya wapiga kura 23,161,440 (asilimia 96.85) ya waliokadiriwa 23,913,184. Haya ni mafanikio makubwa ikitiliwa maanani kuwa Tume ilikabiliwa na upungufu wa rasilimali na ilikuwa kwenye shinikizo kubwa kutoka kwa wadau mbalimbali. Pamoja na kuwa hakuna sheria inayowalazimisha watu kujiandikisha, mwitikio wa watu ulikuwa mkubwa na hivyo kudhihirisha kuwa watu wana mwamko mkubwa kuhusu haki zao za kiraia. Tume ilitumia daftari lililoboreshwa la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2015.

TEMCO inaipongeza Tume kwa kutumia teknolojia ya BVR kuandikisha wapiga kura badala ya mfumo wa awali wa OMR. Matumizi ya teknolojia ya yaliiwezesha Tume kubaini majina 231,955 ya watu waliojiandikisha zaidi ya mara moja, pamoja na mengine 3,870 ya watu wasio kuwa raia wa Tanzania.

TEMCO iliona kuwa zoezi la uandikishaji kwa kutumia teknolojia ya BVR lilichukua muda mrefu na hakukuwa na mbinu za uhakika za kutambua uraia na sifa nyingine za uandikishaji. Pia Watanzania waishio nje ya nchi pamoja na wagonjwa waliolazwa hospitali walikosa fursa ya kuandikishwa.

6.3 Uteuzi ndani ya vyama

Matokeo ya uangalizi wa TEMCO yanadhihirisha kuwa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vingi haukukidhi vigezo vya demokrasia. Njia kuu nne za uteuzi ndani ya vyama zilijitokeza, ikiwemo (i) *uteuzi* (ii) *kutuma maombi* (iii) *kusubiri wanaojitoa na kuhama vyama* (iii) *nusu-demokrasia na nusu-shirikishi* (iv) *demokrasia na shirikishi*. Njia ya uteuzi ilihusisha viongozi wa vyama kuteua watu waliowataka bila kushirikisha watu wengine. Njia hii ilitumia na vyama "vidogo" hasahasa vile visivyokuwa na wabunge na wala madiwani na vilivyo na ofisi Dar es Salaam na mikoa michache tu. Njia ya kutuma maombi ilikuwa ni mbinu mpya iliyotumiwa hasahasa na vyama "vidogo" viliavyoamua kutangaza nafasi za ugombea katika ngazi za majimbo na kata. Njia ya kusubiri waliokatwa na kuhama vyama ilitumika kuwapa nafasi wale waliochujwa na vyama vyao. Njia hii ilitumika na vyama vinavyounda UKAWA na kwa namna fulani ilikandamiza misingi ya demokrasia. Njia ya nusu-demokrasia ilikuwa na chembechembe za ushirikishwaji ingawa viongozi wa vyama walikuwa na uamuzi wa mwisho. Njia ya demokrasia ilitumika na CCM na CUF (hasa Zanzibar) ambapo wanachama walikuwa huru kuchukua fomu za kugombea na kushindanishwa na wengine ndani ya chama katika ngazi tofauti, ikiwemo urais. Uchaguzi hufanywa kwa kutegemea taratibu zilizowekwa na chama.

Hata hivyo, baadhi ya vyama vililazimika kutumia njia zisizokuwa za kidemokrasia za uteuzi kwa kuwa sheria ya uchaguzi haitoi fursa kwa vyama kuungana kwa minajili ya kushinda uchaguzi.

Kwa ujumla, utazamaji wa TEMCO unaonyesha kuwa baada ya miaka 23 ya kuwepo kwake, vyama vya siasa havijaweza kujigeuza kuwa asasi zenye demokrasia na havijaweza kufanya kazi yao ya msingi inayohusiana na uandaaji na ulezi wa viongozi. Kasi yao kuelekea kujenga na kuimarisha demokrasia bado ni ndogo.

6.4 Uteuzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar

Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zina majukumu ya kuteua majina yanayopendekezwa na vyama kwa wagombea wanaosimama katika ngazi mbalimbali. Pia tume zote mbili zina mamlaka ya kusikiliza rufaa dhidi ya uteuzi katika ngazi mbalimbali zinazoletwa na wagombea, msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi au msajili wa vyama vya siasa. Wale wasioridhishwa na uamuzi wa ngazi ya chini huweza kukata rufaa ngazi inayofuata na mpaka ngazi ya taifa.

Katika uchaguzi wa mwaka 2015 wagombea 10 walichukua fomu za uteuzi ndani ya Tume. Hata hivyo ni wagombea nane tu (mwanamke mmoja) ndio waliotimiza vigezo vya uteuzi. Katika ngazi ya ubunge wagombea 1,218 (wanaume 985 asilimia 80.9 na wanawake 233 asilimia 19.1) waliteuliwa na Tume. Uchaguzi wa serikali za mitaa ulikuwa na wagombea 10,879 (wanaume 10,191 asilimia 93.7 na wanawake 679 asilimia 6.3).

Kama inavyotakiwa na sheria ya uchaguzi, Tume ilipokea na kutolea uamuzi rufaa zilizoletwa kwake kwa ama kukubaliana au kupingana na uamuzi wa chini. Kulikuwa na matukio ya wagombea kuwekewa pingamizi katika ngazi za chini na kuwafanya baadhi ya wagombea kupita bila kupingwa. Lakini Tume ilikataa rufaa nyingi za aina hii na kuwarejesha wagombea hawa majimboni kuendelea na uchaguzi. Baadhi ya rufaa zilizosikilizwa na Tume ni zile zilizotoka majimbo ya Tandahimba, Mwanga, Wanging'ombe, Handeni Mjini na Kasulu Mjini. Tume pia ilipokea na kusikiliza rufaa za kata 70. Tofauti na uchaguzi wa mwaka 2010 ambapo wagombea ubunge 16 wa CCM

pamoja na madiwani 500 walipita bila kupingwa, suala la mgombea kupita bila kupingwa halikujitokeza katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Kwa ujumla, Tume ilishughulikia rufaa kwa mujibu wa sheria na wadau wengi waliridhika. Ni muhimu pia kubainisha kuwa idadi ya wanawake walioptishwa na Tume kugombea haitoshi na inaibua maswali mengi kuhusiana na ufanisi wa mikakati ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi kama wagombea.

Tathmini ya watazamani juu ya uteuzi katika majimbo 150 yaliyoangaliwa na TEMCO kati ya 264 inaoneshwa katika Jedwali Namba 1.

Jedwali Namba 1: Tathmini ya uteuzi wa wagombea

Sifa na kielelezo cha uteuzi	**Alama**	**Idadi**	**Asilimia**
Uteuzi wa wagombea uligubikwa na upendeleo mkubwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa Uteuzi umekuwa kama mimba iliyoharibika.	F (0%)	0	0.00
Uteuzi umevurugika au kuborongwa kiasi kwamba inashindikana kwa wadau kuyakubali matokeo ya uteuzi. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani.	E (1-39%)	0	0.00
Uteuzi uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya sheria na kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji na uwepo wa vitisho na upendeleo.	D (40-49%)	5	3.51
Uteuzi uliruhusu ushiriki wa wadau wote (vyama, wagombea, wapiga kura) lakini kukawepo matukio ya vyama vikubwa, au chama tawala, kutokuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi na kutokuadhibiwa kwa hilo na ukawepo upendeleo unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wadau.	C (50-59%)	16	10.53
Uteuzi ambao kwa jumla ni huru na wa haki, lakini bado kuna upungufu ambao unaweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapiga kura).	B (60-69%)	68	45.61
Ni uteuzi safi na wa kiungwana ambao una upungufu wa kawaida usioweza kuathiri matokeo ya uchaguzi.	A (80 – 100%)	61	40.35
Jumla		**150**	**100**

Uchambuzi wa majimbo 150 unaonyesha kuwa kama hali hii ingekuwa hivi majimbo yote, mchakato wa uteuzi ndani ya majimbo 16 (asilimia 10.53) ungechukuliwa kuwa "*huru lakini sio wa haki*"; katika majimbo 68 (asilimia 45.61) uteuzi ungepata cheti cha "*huru na haki wenye walakini*" na katika majimbo mengine 61 (asilimia 40.35) uteuzi ungepata hati ya uchaguzi "*safi, huru na wa haki*".

6.5 Tathmini ya kampeni

Taarifa za watazamaji wa TEMCO zinaonesha mazuri na upungufu kwa namna ambavyo vyama viliendesha kampeni za uchaguzi. Upande wa mazuri unagusia yafuatayo:

i. Kulikuwa na ratiba ya kampeni za wagombea urais ambayo vyama vingi viliifuata. Hata hivyo kuna wakati ililazimu kufanya marekebisho ya hapa na pale;

ii. Ni vyama vitatu tu CCM, CHADEMA/UKAWA na ACT-Wazalendo vilivyoweza kuzindua kampeni zao kitaifa ikiwemo uzinduzi wa ilani zao za uchaguzi;
iii. Ni vyama viwili tu CCM na CHADEMA/UKAWA vilivyovutia mamia ya watu katika mikutano yao ya kampeni ambayo hata hivyo ilitawaliwa na amani na utulivu;
iv. Maafisa wa polisi wenye sare walionekana wakati wa kampeni za urais.

Upande wa upungufu, waangalizi wa TEMCO waligundua yafuatayo:

i. Ingawa kwa ujumla kampeni zilikwenda vizuri, kulikuwa na madai ya mgongano kati ya wafuasi wa vyama viwili vikubwa katika jimbo la Tarime yaliyosababisha kifo;
ii. Kulikuwa na matukio machache ya mikutano ya kampeni kuendelea baada ya saa 12.00 jioni kama inavyotakiwa na kanuni za maadili. Pamoja na hitilafu hii polisi walikuwa wavumilivu na hivyo kuepusha rabsha ambazo zingeweza kutoakea kama wangeingilia kusimamisha mikutano hiyo;
iii. Ingawa ratiba ya kampeni ilikubaliwa kwa pamoja na vyama vyote, kiasi kikubwa haikufuatwa;
iv. Kampeni zilihusisha watu na hisia kuliko asasi (vyama vya siasa) na ilani za uchaguzi;
v. Kulikuwa na tuhuma kuwa vyama viwili vikubwa (CCM na CHADEMA/UKAWA) katika kampeni za urais vilitumia pesa kupita kiwango kilichowekwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Hata hivyo ni vigumu sana kuthibitisha tuhuma hizi;
vi. Vyama vingi vilikuwa dhahiri vikikabiliwa na ukata ukiacha CCM na CHADEMA/UKAWA, hivyo uwanja haukuwa sawa na kuathiri haki katika uchaguzi;
vii. Kulikuwa na matukio katika maeneo machache ya kampeni hasi, ikiwemo kutumia lugha ya kashfa na uchochezi kwenye mikutano;
viii. Kulikuwa na matumizi makubwa ya lugha za asili katika baadhi ya maeneo hasa wakati wa kampeni za madiwani na wabunge, kinyume na vipengele vya sheria ya uchaguzi.

Tathmini ya kampeni za uchaguzi ya watazamaji wa TEMCO inaoneshwa katika Jedwali Namba 2:

Jedwali Na 2: Tathmini ya kampeni za uchaguzi

Sifa na kielelezo cha kampeni	Alama	Idadi	Asilimia
Kampeni ambazo ziligubikwa na upendeleo mkubwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa. Kampeni zimekuwa kama mimba iliyoharibika.	F (0%)	0	0
Kampeni za uchaguzi zimevurugika au kuborongwa kiasi kwamba inashindikana kwa wadau kuyakubali matokeo yake. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani.	E (1 - 39%)	0	0
Kampeni za uchaguzi ziligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya sheria na kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji na uwepo wa vitisho na upendeleo.	D (40 - 49%)	4	2.63
Kampeni za uchaguzi ziliruhusu ushiriki wa wadau wote (vyama, wagombea, wapiga kura) lakini kukawepo matukio ya vyama vikubwa, au chama tawala, kutokuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi na	C (50 - 59%)	16	10.53

kutokuadhibiwa kwa hilo na ukawepo upendeleo unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wadau.			
Kampeni za uchaguzi ambazo kwa jumla ni huru na za haki, lakini bado kuna upungufu ambao unaweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapiga kura).	B (60 - 79%)	88	58.77
Ni Kampeni za uchaguzi safi na za kiungwana ambazo zina upungufu wa kawaida usioweza kuathiri matokeo ya uchaguzi.	A (80 - 100%)	42	28.07
Total		**150**	**100**

Takwimu katika Jedwali Namba 2 zinaonesha kuwa kampeni katika majimbo 16 (asilimia 10.53) zilistahili hati ya uchaguzi "*huru lakini sio haki*"; majimbo 88 (asilimia 58.77) yalipata hati ya uchaguzi *"huru na haki wenye walakini"*; na majimbo 42 (asilimia 28.7) yanastahili hati ya uchaguzi "*safi, huru na haki*".

Watazamaji wa TEMCO hawakutoa taarifa yoyote ambapo mgombea kwa makususi alinyimwa fursa ya kufanya mkutano wa kampeni. Hivyo, tunaweza kuhitimisha kuwa kampeni zilikuwa za amani. Hata hivyo, kulikuwa na upungufu mdogo ambao usingeweza kuathiri ubora wa uchaguzi.

6.6 Siku ya uchaguzi: kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo

Siku ya kupiga kura TEMCO iliweka waangalizi 7,500 kutazama shughuli za siku ya uchaguzi ikiwemo kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo. TEMCO pia ilinufaika na takwimu zilizotokana na Kituo cha Uangalizi wa Uchaguzi (EOC) kilichokuwa chini ya CEMOT ambazo zilionesha kuwa:

i. Vituo 6,080 vya kupigia kura (asilimia 94) vilivyotazamwa vilifunguliwa saa 1.00 asubuhi au kabla; vituo 249 (asilimia 4) vilifunguliwa kuanzia saa 1.31asubuhi-02.00 asubuhi. Ni vituo 115 tu (asilimia 2) ndio vilifunguliwa kuanzia saa 02.01 asubuhi na kundelea.
ii. Kati ya vituo 6,579 vilivyokuwa na watazamaji wa TEMCO/CEMOT vituo 5,921 (asilimia 90) vilikuwa na vifaa vya kutosha vya kupigia kura, ambapo vituo 658 (asilimia 10) vilikuwa na upungufu wa vifaa vya kupigia kura na hasa mihuri.
iii. Katika vituo 1,224 (asilimia 18) kati ya vituo 6,579 ukosekanaji wa majina ulitamalaki.
iv. TEMCO iliona mawakala wa vyama viwili vikubwa CCM na CHADEMA/UKAWA. Kati ya vituo 6,579, CCM kilikuwa na mawakala 6,475 (asilimia 98), CHADEMA/UKAWA kilikuwa na mawakala 6,351 (asilimia 97), na vyama vingine vilikuwa na jumla ya mawakala 4,585 (asilimia 70).
v. Vituo 6,259 (asilimia 95) kati ya 6,579 vilikuwa na askari polisi wenye sare.
vi. Vituo 6,075 (asilimia 92) kati ya 6,579 vilivifika kwa urahisi na watu wenye ulemavu.
vii. Kati ya vituo 5,770 vilivyotazamwa na TEMCO, katika vituo 5,736 (asilimia 99) maafisa wa uchaguzi walihakiki kitambulisho cha mpiga kura.
viii. Dalili au vifaa vya kampeni vilionekana katika vituo 245 (asilimia 4) kati ya vituo 5,770.
ix. kati ya vituo 5,770 vilivyoangaliwa na TEMCO, katika vituo 5,161 (asilimia 89) maafisa uchaguzi walikagua vidole kuangalia dalili za wino usiofutika.
x. Katika vituo 2,492 (asilimia 43) kati ya vituo 5,770, wapiga kura walikuwa kwenye mstari kufikia saa 10.00 jioni ambao ni muda rasmi wa kufunga zoezi la kupiga kura.
xi. Mtu wa mwisho katika mstari alipiga kura kati ya saa 11.00 jioni-1.30 jioni katika vituo 824 (asilimia 43).
xii. Zoezi la kuhesabu kura lilianza mara moja baada ya mtu wa mwisho kupiga kura.

- Vituo 2,206 (asilimia 41) kati ya 5,325 vilivyaongaliwa na TEMCO vilijigeuza kuwa vituo vya kuhesabu kura na kuhesabu kura kulianza kati ya saa 10.30 jioni na saa 11.00 jioni.
- Vituo 1,280 (asilimia 24) kati ya 5,325 vilivyoangaliwa na TEMCO vilijigeuza kuwa vituo vya kuhesabia na kuhesabu ura kulianza baada ya saa 11 jioni.

xiii. Waangalizi wa TEMCO walishuhudia matokeo ya nafasi mbalimbali yakibandikwa nje ya vituo vya kuhesabia kura kama ifuatavyo: urais, 5,038 (asilimia 96); ubunge, 4,887 (asilimia 92); na udiwani, 5,038 (asilimia 96).

xiv. TEMCO ilishuhudia mivutano iliyotokana na madai ya kucheleweshwa kwa matokeo ya uchaguzi katika baadhi ya majimbo ikiwemo Mbagala, Kinondoni, Ubungo, Kibamba, Kawe, Mbozi, Temeke, Simanjiro na Babati na hali ilikuwa mbaya katika baadhi ya majimbo haya na kuleta vurugu.

Waangalizi wa muda mfupi walitakiwa kufanya tathmini ya ujumla ya siku ya uchaguzi kwa kutilia maanani jinsi ambavyo upigaji kura, kuheabu kura na kutangaza matokeo kulivyofanyika. Matokeo ya tathmini yanaoneshwa katika Jedwali Namba 3:

Jedwali Na. 3: Tathmini ya siku ya uchaguzi

Sifa na kielelezo cha upigaji kura	**Alama**	**Idadi**	**Asilimia**
Upigaji kura na kuhesabu kura uligubikwa na upendeleo mkubwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa. Upigaji kura na kuhesabu kura zimekuwa kama mimba iliyoharibika.	F (0%)	1	0.01
Upigaji kura na kuhesabu kura umevurugika au kuborongwa kiasi kwamba inashindikana kwa wadau kuyakubali matokeo yake. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani.	E (1-39%)	0	0
Upigaji kura na kuhesabu kura uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya sheria na kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji na uwepo wa vitisho na upendeleo.	D (40-49%)	10	0.13
Upigaji kura na kuhesabu kura uliruhusu ushiriki wa wadau wote (vyama, wagombea, wapiga kura) lakini kukawepo matukio ya vyama vikubwa, au chama tawala, kutokuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi na kutokuadhibiwa kwa hilo na ukawepo upendeleo unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wadau.	C (50-59%)	122	1.62
Upigaji kura na kuhesabu kura ambao kwa jumla ni huru na za haki, lakini bado kuna upungufu ambao unaweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapiga kura).	B (60-69%)	1612	21.49
Ni Upigaji kura na kuhesabu kura safi na wa kiungwana ambaoo una upungufu wa kawaida usioweza kuathiri matokeo ya uchaguzi.	A (80 – 100%)	5755	76.74
Jumla		**7500**	**100**

Kama inayoonekana katika Jedwali Namba 3 waangalizi 5,755 (asilimia 76.74) wanaonesha kuwa siku ya uchaguzi ilikuwa na upungufu kidogo ambao haukuathiri upigaji kura na

utangazaji matokeo. Kwa sababu hii upigaji kura na kuhesabu matokeo kunastahili hati ya uchaguzi ambao ni "*msafi, huru na wa haki*". Upigaji kura na kuhesabu kura katika vituo 1,612 (asilimia 21.5) unapewa hati ya "*huru na wa haki wenye walakini*" ambapo vituo 122 (asilimia 1.62) unapata hati ya uchaguzi "*usio huru na wala wa haki*".

7. Tathmini ya ujumla ya uchaguzi wa mwaka 2015

Baada ya kukusanya habari na takwimu, watazamaji wa muda mrefu wa TEMCO walitakiwa kutathmini na kuamua bila upendeleo juu ya namna mchakato mzima wa uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2015 ulivyoendeshwa. Matokeo yanaoneshwa katika Jedwali Namba 4:

Jedwali Namba 4: Tathmini kuu ya mchakato wa uchaguzi

Sifa na kielelezo cha uchaguzi	**Alama**	**Idadi**	**Asilimia**
Uchaguzi uligubikwa na upendeleo mkubwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa. Uchaguzi umekuwa kama mimba iliyoharibika.	F (0%)	0	0
Uchaguzi umevurugika au kuborongwa kiasi kwamba inashindikana kwa wadau kuyakubali matokeo yake. Ni kama mwanafunzi aliyefeli mtihani.	E (1-39%)	0	0
Uchaguzi uligubikwa na dosari nyingi kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya sheria na kanuni, udhaifu wa kiuendeshaji na uwepo wa vitisho na upendeleo.	D (40-49%)	0	0
Uchaguzi uliruhusu ushiriki wa wadau wote (vyama, wagombea, wapiga kura) lakini kukawepo matukio ya vyama vikubwa, au chama tawala, kutokuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi na kutokuadhibiwa kwa hilo na ukawepo upendeleo unaoathiri ushiriki au mafanikio ya baadhi ya wadau.	C (50-59%)	5	3.51
Uchaguzi ambao kwa jumla ni huru na wa haki, lakini bado kuna upungufu ambao unaweza kuathiri sudi za baadhi ya wadau (vyama, wagombea, wapiga kura).	B (60-69%)	67	44.74
Ni Uchaguzi safi na wa kiungwana ambaoo una upungufu wa kawaida usioweza kuathiri matokeo ya uchaguzi.	A (80%+)	78	51.75
Jumla		**150**	**100**

Tathmini ya ujumla inaonesha kuwa mchakato mzima wa uchaguzi katika majimbo matano (asilimia 3.51) unastahili kutunukiwa hati ya uchaguzi "*huru lakini sio wa haki*", ambapo shughuli za uchaguzi katika majimbo 67 (asilimia 44.74) unachukuliwa kuwa "*huru na wa haki wenye walakini*", wakati uchaguzi katika majimbo 78 (asilimia 51.75) unastahili hati ya uchaguzi "*safi, huru na wa haki*".

Ukichukuliwa kwa mapana na marefu yake, uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2015 unastahili hati ya uchaguzi "*safi, huru na wa haki*". Hata hivyo, ikizingatiwa hisia za kutoridhishwa na

wasiwasi wa wadau wengi wa uchaguzi kuhusiana na uhuru wa Tume, sheria na kanuni pamoja na upungufu wa hapa na pale ulioainishwa na watazamaji, TEMCO haiwezi kutoa hati hiyo. Na kwa hiyo, TEMCO inatoa hati ya uchaguzi "***Huru na wa Haki Wenye Walakini***" kwa uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2015.

8. Uchaguzi wa Zanzibar

TEMCO ilipokea kwa mshituko na mshangao uamuzi wa kufuta matokeo ya uchaguzi uliotangazwa na mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa alichoelezea kuwa ni "ukiukwaji na uvunjaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi". Mifano halisi iliyonukuliwa na mkuu wa Tume ni vitisho kwa wapiga kura hasa kwenye maeneo ambako ni ngome za vyama, kupoka mamlaka ya Tume juu ya utangazaji wa matokeo ya kura ya urais, tofauti zilizofikia hatua ya wajumbe wa Tume kutwangana makonde, na idadi ya wapiga kura katika baadhi ya vituo kuzidi ile ya waliojiandikisha, hasa Pemba.

Kulikuwa na watazamaji wa uchaguzi 22 wa muda mrefu na 704 wa muda mfupi wa TEMCO huko Zanzibar. Waangalizi wa uchaguzi wa muda mrefu waliwasili zanzibar siku 43 kabla ya uchaguzi. Watazamaji wa muda mrefu na muda mfupi kwa pamoja waliangalia michakato ya siku ya uchaguzi ikiwemo kupiga kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo na yaliyojiri mara tu baada ya matokeo kutangazwa. Taarifa zao za awali zinaonesha kuwa shughuli zote za kabla ya uchaguzi zilifanyika kwa weledi na kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu kwa amani na utulivu. Inashangaza kuwa uamuzi wa kusitisha uchaguzi ulitolewa wakati tayari kura zikiendelea kuhesabiwa na matokeo kutangazwa.

Vilevile, TEMCO ilishtushwa na tamko ambalo halikusainiwa lililoandikwa kwa Kiingereza na kutolewa kwa umma na CUF tarehe 26 Oktoba 2015 likiwa na kichwa cha habari kilichosomeka "CUF yashinda uchaguzi wa kihistoria Zanzibar" au "the Civic United Front Wins Historic Victory in Zanzibar Election". Sehemu ya tamko hilo ilisomeka kama ifuatavyo:

> Kufikia saa 3.30 asubuhi hii, Maalim Seif Hamad, mgombea urais wa Civic United Front zanzibar, alikuwa amepata kura 200,077 dhidi ya mshindani wake wa karibu Dk. Ali Mohamed Shein wa CCM mwenye kura 178,363. Hii inaifanya CUF kuwa na wingi wa kura 21,714—asilimia 52.87 dhidi ya asilimia 47.13… Watu wa Zanzibar wamesema… Hakuna ubishi kuwa Maalim Seif ameshinda uchaguzi wa urais Zanzibar na kwamba chama tawala kimeshindwa kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1977.
>
> [As of 9.30 this morning, Maalim Seif Hamad, the Presidential candidate of the Civic United Front in Zanzibar, had secured 200,077 votes against his rival Dr. Ali Mohamed Shein of the CCM with 178,363 votes. This constitutes a majority for the CUF of 21,714 votes—52.87% against 47.13%. …The people of Zanzibar have spoken. …There is now no question that Maalim Seif has won the presidential election in Zanzibar and that the ruling party has been defeated for the first time since 1977].

Uamuzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar na tamko la CUF vinaacha maswali mengi. Uamuzi wa Tume a tamko la CUF vimesababisa mijadala mikali kati ya wadau na kuleta dukuduku kati ya vyama, wagombea urais na waangalizi wa ndani na nje. TEMCO inaendelea kuwa na shauku ya kufuatilia mwenendo wa uchaguzi Zanzibar, na hivyo:

i. Inaisihi sana Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kufikiria upya uamuzi wake kwa lengo la kufikia chaguzi huru, haki na za kuaminika ili kuimarisha amani na

mshikamano katika moyo wa Maridhiano ambayo yaliwezesha kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mwaka 2010;

ii. Inavisihi vyama vya siasa na wagombea urais kuheshimu mamlaka ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na sheria za uchaguzi;

iii. Inatoa wito kwa wadau na wachezaji wakuu wa uchaguzi hasahasa CUF na CCM kuendelea kuwa watulivu na kujiepusha na matumizi ya nguvu na kuacha kutoa kauli ambazo zinaweza kuchochea au kuongeza mivutano na migogoro isiyo na tija;

iv. Inazisihi pande zinazodai haki katika mashauri yanayohusiana na kufutwa kwa uchaguzi wa Zanzibar kufiata taratibu zilizopo za kisheria ili kulinda amani, uhuru na usalama;

v. Inauomba uongozi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikiria kutafuta njia na namna ya kusuluhisha mgogoro huu ambao unaweza kuvuruga amani sio tu ya Zanzibar lakini pia Tanzania Bara;

vi. Inawaomba watu wote wanaopenda amani ikiwemo jumuiya ya kimataifa, washirika wa maendeleo, viongozi wa dini, asasi za kiraia,marais wastaafu, vyombo vya habari, na wananchi wote wenye kuwajibika kuchangia katika kusaka suluhu ili muafaka upatikane haraka iwezekanavyo;

vii. Inawasihi makamishna wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuwajibika kutokana na yaliyotokea na kusababisha uchaguzi kufutwa. Vilevile mamlaka za uteuzi zichukue hatua za kinidhamu dhidi ya maafisa wa Tume kwa dhima yao katika ufutaji wa uchaguzi.

9. Hitimisho na mapendekezo

9.1 Hitimisho

Kwa ujumla, uchaguzi wa Tanzania wa mwaka 2015, ukiacha ule wa Zanzibar, ulisimamiwa vizuri na matokeo yake yanaakisi matakwa ya wapiga kura. TEMCO: (i) inawapongeza wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza haki yao ya kiraia kwa kujitokeza kwa wingi katika zoezi la BVR, kuhudhuria mikutano ya kampeni na kupiga kura pamoja na kuimarisha ulinzi, usalama na amani kwa kipindi chote cha uchaguzi; (ii) inaipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, makamishna na maafisa) kwa kutimiza wajibu wao kwa weledi, uchapakazi na uzalendo kwa mujibu wa sheria; (iii) inawapongeza wagombea wote (walioshinda na walioshindwa) wa chaguzi za Jamhuri ya Muungano, uchaguzi wa Zanzibar na chaguzi za serikali za mitaa pamoja na wadau wengine zikiwemo asasi za kiraia, vyombo vya habari, asasi za kidini na washirika wa maendeleo kwa kuwezesha uchaguzi kwa namna moja au nyingine.

TEMCO inawapongeza wanawake hasa mgombea mwenza wa urais wa CCM na mgombea urais wa ACT-Wazalendo. Pia wagombea wengi wanawake waliosimama katika nafasi za ubunge na udiwani walithibitisha uwezo wao kwa kushinda katika majimbo ambayo yalikuwa yakishikiliwa na wanaume. TEMCO inafahamu kuwa uchaguzi uliahirishwa katika majimbo na kata nyingi kwa sababu ya kufariki kwa wagombea. Waliaga dunia kabla ya kutimiza ndoto na malengo yao ya kisiasa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Azilaze Roho Zao Mahali Pema Peponi.

TEMCO inapenda kuwapongeza wagombea walioshinda uchaguzi katika ngazi mbalimbali, na kwa namna hiyohiyo washiriki wote hasa wale waliokuwa chini ya mwavuli wa UKAWA kwa kuleta chachu na ushindani mkubwa katika uchaguzi na kwa kweli waliufanya kuwa uchaguzi wa kihistoria. Wakati joto la kisiasa likishuka na vumbi la uchaguzi likiendelea kutulia, washindi na walioshindwa watambue kuwa uchaguzi wa amani ulikuwa ni matokeo ya tunu za taifa zinazowaunganisha Watanzania zikiwemo uvumilivu wa mawazo tofauti, moyo wa umoja, amani na utulivu na hasa hamu ya Watanzania ya kuendelea kuimarisha demokrasia.

9.2 Mapendekezo

Kwa kutilia maanani matokeo ya uangalizi wa uchaguzi, TEMCO inapenda kutoa mapendekezo kwa wadau mbalimbali wanaohusika na usimamizi wa uchaguzi ili kuboresha chaguzi za Tanzania.

9.2.1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Serikali inashauriwa kufikiria uwezekano wa kufanya maboresho makubwa katika uchaguzi kwa minajili ya:

i. Kuongeza imani na matumaini ya wadau wa uchaguzi kwa wasimamizi wa uchaguzi hasa kwa kuangalia upya uteuzi wa makamishna na mkurugenzi wa uchaguzi pamoja na haja ya Tume kuwa na maafisa wake yenyewe katika ngazi zote;
ii. Kurekebisha au kupitia upya sheria ya uchaguzi ili kuruhusu mgombea binafsi, kupinga matokeo ya urais mahakamani na kuruhusu Watanzania wanaoishi nje ya nchi kupiga kura;
iii. Kuanzisha na kutekeleza mpango kamambe wa kitaifa wa elimu ya uraia ambao utatoa dira ya utoaji wa elimu ya mpiga kura;.
iv. Kuchukua hatua za kuimarisha asasi za makuzi ya vijana kwa nia ya kurekebisha tabia zao ili kuwafanya wawe na subira, wastahimilivu na wawajibikaji;
v. Kuchukua hatua zitakazosaidia utendaji wa mitandao ya kijamii wakati wa uchaguzi ili kuepuka upotoshaji wa habari na kuharibu mchakato wa uchaguzi;
vi. Ni muda muafaka kwa serikali kufikiria kuifanyia marekebisho Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuwa na kipengele kitakachoruhusu vyama vya siasa kuunda umoja/ushirika/muungano kwa minajili ya kushiriki katika uchaguzi.

9.2.2 Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kama ilivyogusiwa awali, TEMCO imeridhishwa na utendaji wa Tume kwa upana wake wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015. Mapendekezo yafuatayo yanaelekezwa kwa Tume:

i. Kwa kutumia mtaji wa uzoefu waliojikusanyia na uwezo na umahiri ulioonyeshwa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015, Tume ifikirie kuanza maandalizi ya upigaji wa kura ya maoni kwa Katiba Inayopendekezwa ikizingatiwa kuwa daftari la kudumu la wapiga kura limekwishaboreshwa;
ii. Tume iendelee kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura kama ilivyobainishwa na sheria. Hii itasaidia hata kwa wale ambao majina yao yalikosekana wakati wa kupiga kura kuingizwa katika daftari.

9.2.3 vyama vya siasa

Vyama vya siasa ni wadau wakuu wa uchaguzi. TEMCO inapendekeza yafuatayo kwa vyama vya siasa:

i. kuheshimu na kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu;
ii. kujifunza kuelekeza malalamiko yao katika njia muafaka kama vile mahakama;

iii. kuchukua hatua za kujenga na kuimarisha demokrasia ndani ya vyama has wakati wa uteuzi wa wagombea;
iv. kujifunza kukubali matokeo ya uchaguzi badala ya kupinga hata baada ya kushindwa;
v. kuchukua hatua ambazo zitawahamasisha na kuwawezesha wanawake kushiriki katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi;
vi. kujiepusha na kupoka mamlaka ya Tume za uchaguzi; na,
iii. kujitahidi kuwa asasi zinazojifunza na zenye uwezo wa kujiendeleza, kuwa na misingi ya itikadi ambayo inaweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja mpaka kingine na kujiepusha na kasumba ya kutukuza kiongozi mmoja.

10. Shukrani

Kwa niaba ya asasi 172 zinazounda TEMCO (Tanzania Election Monitoring Committee), uongozi wa REDET, asasi kiongozi ya TEMCO, ingependa kutoa shukrani zake za dhati kwa hawa wafuatao:

i. kutoa shukrani za dhati kwa Watu wa Marekani, kupitia Shirika lake la Maendeleo, yaani USAID, kwa kutoa pesa za kuendeshea programu ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (Observation of Tanzania 2015 Electoral Processes—OTEP). Pasi na msaada huu usiokuwa na masharti, kazi hii ya uangalizi wa uchaguzi isingewezekana.
ii. kutammbua mchango wa waangalizi 180 wa muda mrefu na 7,350 wa muda mfupi kwa kufanya kazi zao kwa umakini, bila upendeleo na kwa weledi.
iii. kuushukuru uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuendelea kuisaidia TEMCO kwa hali na mali, kutoa ofisi, na kuongeza uhalali na heshima ya TEMCO kama kilivyofanya tangu awali. TEMCO ilifaidika sana na wigo mpana wa ujuzi na maarifa uliopo ndani ya Chuo Kikuu.
iv. kutoa shukrani kwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa kuridhia TEMCO kufanya shughuli ya utazamaji wa uchaguzi tokea wakati wa BVR mpaka michakato mingine iliyofuatia. Vilevile TEMCO inatoa shukrani za dhati kwa waratibu wa chaguzi wa mikoa, wasimamizi wa uchaguzi na maafisa wengine wa uchaguzi majimboni.
v. kutambua ushirikiano wa Legal and Human Rights Centre (LHRC), asasi kiongozi ya TACCEO, kwa kuanzisha CEMOT (Coalition on Election Monitoring and Observation in Tanzania) iliyosimiamia kituo cha uangalizi wa uchaguzi kilichokuwa kitovu cha matumizi ya Tehama katika kuangalia uchaguzi.
vi. kushukuru na kutambua msaada wa pesa kutoka kwa ubalozi wa Denmark, Ubalozi wa Canada, na OSIEA (Open Society Initiative for East Africa) uliowezesha CEMOT kuendesha shughuli zake.
vii. kushukuru msaada wa pesa ukiotolewa na NDI (National Democratic Institute) ulioiwezesha TEMCO kuboresha kwa kiasi kikubwa mbinu za kukusanya taarifa kwa kutumia TEHAMA.
viii. kuwashukuru wadau wengine wa uchaguzi vikiwemo vyama vya siasa, wagombea, waangalizi wa kimataifa, na wapiga kura wa Tanzania kwa kubadilishana uzoefu na maarifa kuhusu uangalizi wa uchaguzi.